

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

**SHULE YA SEKONDARI  
GIDAHABABIEG,  
S.L.P 233,  
KATESH – HANANG.  
1/12/2022  
Tell: 0686636456**

**Kumb.Na. GSS/ ADIMIN VOL 01/K1. 2023  
MZAIZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI**

.....  
**SHULE YA MSINGI .....**  
**S. L. P .....**  
**KATESH – HANANG’**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GIDAHABABIEG**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2023 shule ya sekondari Gidahababieg iliyopo katika Kata ya Gidahababieg kitongoji Cha lambo.

Muhula wa kwanza masomo yanaanza tarehe 9.01.2023 unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe 9.01.2023– 13.01.2023

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

- ❖ Sare ya shule hii ni suruali ya Kijivu shati nyeupe kwa wavulana na sketi ya kijivu blauzi nyeupe kwa wasichana.
- ❖ Rangi ya hijab ifanane na sare za shule.

**MAELEZO:**

- ❖ **SKETI>Kijivumarinda 12, mkanda wa wastani. Pair 02. Pindo la chini wastani lisiwe dogo.**
- ❖ **SURUA kijivu mifuko** ya pembeni “V” yenyeye kifungo mfuko wa nyuma – pair 2
- ❖ **VIATU>** vyeusi vya kamba, visigino vifupi pair2
- ❖ **SOCKSI>** Khaki (Wavulana), nyeupe (wasichana) – pair2
- ❖ **SWEATER>** la kijivu(wasichana) na (wavulana) shingo V iliyopimwa vema pair 2 (wote).
- ❖ Sare ya michezo kwa shule hii ni raba, Trucksuti ya Dark Blue (Ni lazima)

N.B Aje na SHILINGI 11000(Elfu kumi na moja) kwa ajili ya tishert ya shule yenyeye nembo ya shule (ni lazima) tshert ya shule atai kuta shulenii.

- 2.2 Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu, counter books Q3 kwa masomo yote 9 na sio madaftari madogo (**hayaruhuswi**) na rimu paper 1 (A4) kwa mwaka zisiwe za mistari.(rim paper Ni lazima kila mwanafunzi)
- 2.3 Chakula cha wanafunzi wa kutwa mahindi debe 3 kwa mwaka, maharage debe 2 kwa mwaka na Tshs. 60,000/= kwa mwaka.
- 2.4 Vifaa vya usafi **slesha, mopa, mifagio, ndoo ndogo, chelewa, mifagio ya soft broom na jembe.**

### **3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

#### **3.1 MAMBO YAKUZINGATIA**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenyе dhamana ya Elimu nchini naOfisi ya Rais – TAMISEMI yenyе jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu. Kama mwanafunzi unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa vizuri mara baada ya kuripoti shuleni:

- I. Heshima kwa Viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- II. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- III. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio baada ya vipindi vya darasani (preparatrion)
- IV. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyngine utakazopewa;
- V. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- VI. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- VII. Kuva sare ya shule kikamilifu wakati wote unapotakiwa;
- VIII. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- IX. Kutunza mali za Umma na mali binafsi.
- X. Ni lazima mwanafunzi ahudhurie shule siku zote 195 kwa mwaka na kwa masomo yote kwa siku. **UTORO** wa shule/ vipindi ni **MWIKO**. Mzazi kama kuna shida tafadhali toa taarifa shuleni.

#### **3.2 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE**

- Wizi
- Uasherati na ushoga
- Ubakaji
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
- Kupigana au kupiga
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- Kudharau bendera ya Taifa
- Kuwa mjamzito, kupata mimba au kusababisha mimba
- Kutoa mimba
- Kuoa au kuolewa
- Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Kuwa na simu ya mkononi

**MUHIMU: IKIWA MWANAO ANALOTATIZO LA KIAFYA UJE NA TAARIFA TOKA KWA DAKTARI**  
Fomu kwa ajili ya kujaziwa na daktari utaikuta shuleni pamoja na fomu za kukiri kujungu na shule hii

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

.....  
**HAWA O. MSANGI  
MKUU WA SHULE  
Tell: 0686636456**